MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 8 TOLEO 29

MACHI 04, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

MAKALA MAALUM

TUKUBALI AU TUPINGE

HAPANA DOWANS!



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri



Na. Fred Katunzi



Fundi Umeme

Makala zilizokuwa ziendelee wiki hii zitaendelea wiki ijayo hususan suala la vitambulisho vya taifa.

Kutokana na kupamba moto kwa mradi wa Dowans tunalalazima kurudia tena suala hili la Dowans ambalo tulisema wazi kuwa kwa namna yoyote ile Dowans watajaribu kulipwa. Msimamo tunaochukua hapa si msimamo dhidi ya Waziri Ngeleja kama Ngeleja bali tunachukua msimamo huu kutokana na kile tunachoamini kuwa ni vipaumbele vilivyogeuzwa.

Katika taarifa yetu ya mwaka tumesema kuwa kinachotuongoza mwaka huu ni msimamo wa "kutoka kulalamika kuelekea kuhamasika" Tunatambua kuwa tuna uamuzi aidha wa kukaa kimya, au kusema, kuangalia au kutenda, kukubali au kukataa. Katika makala hii tumechukua msimamo wa kukataa hoja zinazotolewa kuhusu kuhalalisha ununuzi wa majenereta ya Dowans.

Baada ya kumsikiliza Waziri wa Nishati na Madini kwa kirefu katika mahojiano yake na Mwanakijiji juzi na baada ya kufanya tafakuri ya kina iliyoenda sambamba na kusikiliza hoja mbadala zina-

HOJA YA MWANAKIJIJI

Walipoamua kununua ndege ya Rais kwa bilioni 50 tuliwapinga, walisikia mapingamizi yetu wakapuuza wakanunua; tukayaona

Walipotaka kunua rada ile ya kijeshi kwa bilioni 40 tuliwapinga, walitusikia, wakatupuuza; tukayaona.

Walipoamua kujenga minara ya Benki Kuu tuliwapinga na kuwahoji, walitusikia, wakatupuuza; tukayaona.

Ilipokuja Richmond na Airbus yote tuliyasema, wakatusikia na wakapuuza na tukayaona.

Sasa tunaambiwa "wameokoka"! Kwamba wanajua kilicho bora na ya kuwa wana uzalendo. Tunawaambia "Hapana Dowans". Wamesikia, watatupuuza, na kutudharau. Na sisi tutaona! Wasije kusema tunapinga maendeleo!

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!**

Ndani ya Toleo Hili

Sema hapana Dowans	1-5
Tahariri	1
Hapana Dowans	2
Hapana Dowans	3
Hapana Dowans	4
Da'Jessy: Tukishawataja?	5
Picha, Katuni na Maoni	6

TUWAAMBIE "HAPANA DOWANS"

zotolewa na watu mbalimbali wakiwemo wabunge mashuhuri kama Mhe. Zitto Kabwe (Kigoma Kaskazini-CHADEMA), Mhe. Harrison Mwakyembe (CCM-Kyela) na Mhe. William Shelukindo (CCM-Bumbuli) tumeona ni lazima tuchukue msimamo ambao tunaamini kwa muda mrefu ujao utakuwa na maslahi makubwa zaidi kwa taifa kuliko tatizo la muda mfupi uliopo.

Msimamo wetu ni wa kupinga kwa nguvu na kwa kauli moja isiyo na utata jaribio na mpango wowote wa serikali kununua majenereta ya umeme kutoka kwa kampuni ya Dowans kama ilivyopendekezwa na kupigiwa debe na uongozi wa Tanesco, Wizara, baadhi ya wabunge. Tunakataa kabisa kwa Watanzania kuendelewa kuchukuliwa kwa dharau, au kuonwa kuwa hatuitakii nchi mema au hatuelewi uharaka au ulazima hali ya nishati nchini.

Msimamo wetu huu tunauchukua kwa maumivu makubwa kwa sababu tunatambua wazi suala la nishati ni muhimu sana kwa taifa na maendeleo ya nchi yoyote ile. Tunatambua vile vile kwamba Taifa letu liko katika wakati ambapo hatuwezi kufanikiwa pasipo kuwa na chanzo cha kudumu na cha kuaminika cha nishati. Tunatambua katika kuchukua msimamo tunaweza kusimama peke yetu kama manabii wa zamani waliotengwa na jamii zao kutokana na ujumbe wao kutokuwa wa kupendeza kwa watawala.

Ni kwa sababu hiyo basi tunajua gharama ya kuchukua msimamo usio na umaarufu hasa kwa kuzingatia suala nyeti kama la nishati. Hata hivyo wakati mgumu unahitaji maamuzi magumu vile vile.

Tunazo sababu kadhaa za kupinga ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme ambayo inauzwa na kampuni ya Dowans. Tunazianisha sababu hizo kama ifuatavyo.

1. **Tatizo la nishati Tanzania haliwezi kuendelea kushughulikiwa kwa vipande vipande.**

Kwa muda mrefu sasa tumeona serikali inavyoshughulikia tatizo la nishati. Kwa mtazamo wetu tunaweza kusema pasipo shaka kuwa serikali haina nia ya dhati na kusudio la kweli la kuondoa tatizo la nishati ya umeme nchini. Kwa miongo kadhaa sasa suala la nishati limekuwa likishughulikiwa kwa kibaba.



Dr. Idris

Leo jenereta, kesho jenereta jingine, keshokutwa bwawa dogo la maji, na mtondogoo mpango wa bwawa jingine la kuzalisha umeme. Endapo tutaangalia jinsi serikali inavyoshughulikia tatizo hili la nishati tunaweza kuamini mambo ambayo si ya kweli. Kwanza, tunaweza kudhania kuwa Tanzania kuna tatizo la vyanzo vya nguvu za umeme, na pili kwamba Tanzania kuna tatizo la fedha za kuendeleza vyanzo vya umeme vilivyopo na ya kuwa kulitatua mara moja na daima tatizo la umeme nchini nchini ni jambo ambalo haliwezekani katika kizazi chetu. Yote hayo mawili au matatu hayana msingi katika ukweli.

Ukitembelea tovuti ya Tanesco (http://www.tanesco.com) utaona sehemu inayozungumzia mpango mkuu wa nishati (master plan) inaonesha miradi mbalimbali iliyoko mbioni ambayo inaonesha vile vyanzo ambavyo tayari vinajulikana kwa uwezo wa kutengeneza nguvu ya umeme. Miradi hiyo kama ingetekelezwa yote ingeweza kuongeza kwenye gridi ya taifa siyo chini ya 660MW za umeme.

Kuelewa umuhimu wa hilo watanzania watambue kuwa vyanzo vya maji (hydropower plants) ambavyo tayari vinazalisha umeme sasa hivi yaani Kidatu, Hale, Pangani, Nyumba ya Mungu, Kihansi, na Mtera, vyanzo hivyo vyote vinauwezo wa kuzalisha kiasi cha 561MW. Ukiongozea na vyanzo vingine vya kukodisha au kununua kutoka wazalishaji huru wa umeme tunapata karibu 930MW

Hii ina maana ya kwamba endapo tungeamua kushughulikia kwa ujumla kuendeleza vyanzo vilivyopo vya maji tu kwa uharaka ambao tunaambiwa upo, tungeweza kuongeza kwenye gridi ya taifa zaidi ya mara mbili ya uwezo wa umeme ambao tayari unapatikana! Kwa maana ya kwanza kungekuwa hakuna haja ya IPTL, Songas, Richmond wala Dowans!

Tunachokiona hata hivyo ni utatuzi wa tatizo la nishati kwa vipande vipande. Hakuna sera madhubuti yenye kutaka kuondoka na tatizo la nishati mara moja na daima na matokeo yake wanasiasa wetu wanakuja kila mwaka na "kamradi" kengine ka nishati kama vile wanatupimia umeme kwa kibaba.

Kwa sababu hii ya kwanza tunapinga kununua vijenereta vya Dowans!

2. **Uwezo wa maporomoko ya Stielgers chini ya RUBADA wa 2100MW**

Katika ya miradi ambayo hatuisikii kabisa ni maporomoko ya Stielgers ambayo kwa watu wengi hata jina labda linaweza kuwa halifahamiki. Mradi huu uliangaliwa na kufanyiwa upembuzi yakinifu karibu miaka thelathini iliyopita. Mradi huu uko chini ya Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Mto Rufiji (RUBADA) na wadau wengine ikiwemo serikali yetu.

Mradi huu haukuendelezwa miaka hiyo kwa sababu moja kubwa kwamba mahitaji ya umeme ya nchi hata eneo letu hayakuwa makubwa kiasi cha kulazimu kujenga bwawa hili. Kama unavyoona mradi huu una uwezo (kama ukijenga kwa kiwango chake cha juu kabisa) wa kutoa megawati 2100 za umeme. Hii ni karibu mara nne ya uwezo wa sasa wa mabwawa yote nchini na kwa hakika ungesababisha miradi ile mingine tuliyoitaja hapo juu kutokuwa ya ulazima wowote.

Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa ni dola bilioni 2. Kiasi hicho kinaweza kuonekana kuwa ni kikubwa mno. Hata hivyo ukichukuliwa kuwa katika Benki Kuu kati ya miaka miwili Tanzania imepoteza kimazingaombwe dola karibu bilioni moja ambazo hadi hivi sasa hakuna juhudi za kweli ya kuzipata imefanyika!

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

Ukichukulia na ripoti ambayo imetoka hivi majuzi toka Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ambapo wamesema kuwa Tanzania inapoteza karibu asilimia 20 ya fedha za bajeti kwenye mambo ya kifisadi utaona kuwa siyo tu tuna uwezo wa kifedha wa kufadhili mradi huu mkubwa ambao utaondoa kabisa na kufanya tatizo la umeme kuwa ndoto bali pia tuna uwezo wa kugeuza maeneo mengine ya vimiradi vidogo vidogo kuwa ya burudani na utalii bila kuyaharibu kwa mitambo na mashine mbalimbali.

Siyo sisi tu tunaoupigia debe mradi huu. Mbunge wa Makete Mhe. Dr. Binilith Mahenge alisema hivi Bungeni "Kimsingi mradi huu kama utachukua njia ya mkato kutoka Chalinze ni kilomita 165 tu unafika kwenye huu mradi. Mheshimiwa Spika, nadhani tulishindwa kufanya yale maamuzi ama ni kwa sababu ya mashinikizo ya wenzetu wakitumia kigezo cha mazingira lakini ukweli ni kwamba walitushinikiza wakati hata wao wenyewe mpaka tunavyoongea sasa hivi wameshindwa kusaini Mikataba ya Kyoto. Sasa nadhani haya ndiyo yaliyotufikisha mahali mpaka tukajikuta tuna matatizo ya umeme na tukaanza kutafuta vitu gani viweze kutusaidia."

Tunafahamu kuwa Rais Kikwete alipokea taarifa ya mpango wa RUBADA kuialika kampuni toka Canada ya Energem kuwa mbia wake na hakuoneshwa kufurahishwa nayo. Tunaamini kuwa wakati umefika kwa uongozi wa kuthubutu, wenye maono ya mbali na wenye utayari wa kuanzisha mradi mkubwa kabisa wa nishati katika eneo letu la Afrika kuanza kutekelezwa. Tunangoja nini?

Sababu hii inatufanya tuupinge mradi wa Dowans!

3. Dowans wameshiriki tayari kwenye mradi wa kifisadi kwanini tuwazawadie tena?

Kwanza tukumbuke kuwa kampuni ya Dowans tayari imeshalipwa mabilioni ya shilingi. Hata ukiondoa fedha tunazowadai kati ya bilioni 8-10 bado wameshajipatia mabilioni ya fedha za Watanzania. Cha kukatisha moyo ni kuwa wote tunajua kuwa kuingia kwa kampuni hiyo hapa nchini tayari kuligubikwa na wingu la ufisadi.

Kampuni hii iliingia kwa haraka kuchukua nafasi ya kampuni ya Richmond ile kampuni ya kifisadi ambayo ilikataliwa na kuumbuliwa na Kamati ya Teule ya Bunge chini ya Dr. Mwakyembe. Kuingia kwake kunashangaza kama tutakavyoona hapa.

a. Kwa mujibu wa Dr. Idris Rashid ni kuwa kampuni hiyo iliingia nchini ikiwa imeandikishwa huko Costa Rica ambako ilianzishwa kwa mtaji wa dola 100!! (dola mia moja). Hayo aliyasema yeye mwenyewe mwishoni mwa mwezi Juni mwaka jana (2008) alipozungumza na waandishi wa habari. Hata hivyo uchunguzi wote uliopo hadi hivi sasa na usio na shaka umeonesha kuwa kampuni hiyo ni ya kutoka Uarabuni ikimilikiwa na familia ya kina Al-Adawi huku watu watatu wakitajwa kuwa ndiyo wamiliki wote wakiwa ni raia wa Falme za Kiarabu. Kwanini kuna tofauti hii? Iweje leo Mkurugenzi yule yule ambaye aliliambia taifa kuwa kampuni hii inatoka Costa Rica leo tuweze kumuamini anapotuambia kuwa hatuna uchaguzi isipokuwa kununua toka Dowans?

b. Habari za ndani ambazo ni za kuaminika zinaonesha uhusiano wa karibu sana kati ya Mbunge wa Igunga Mhe. Rostam Aziz na familia ya Al-Adawi na inadaiwa yeye mwenyewe ni mwekezaji aidha katika kampuni ya Dowans Holdings au makampuni mengine ya familia hiyo. Hilo peke yake halitoshi kutushtua lakini kinachotushtua ni kuwa Dr. Idris Rashid na Waziri William Ngeleja wote wawili wawili kwa wakati mmoja wamefanya kazi chini ya Rostam akiwa mwenye hisa ya asilimia 19 kwenye kampuni ya Vodacom. Ngeleja akiwa ni wakili na Dr. Idris Mkurugenzi. Je yawezekana hawa wawili siyo watu sahihi kuupigia debe mradi huu?

c. Serikali imeithibitisha kuwa kampuni ya Dowans kuingia kwake mkataba na Richmond hakuna kwa maslahi ya taifa. Ukirejea ripoti ya wanasheria wa Bunge ambao walipitia mikataba yote ya Tanesco utaona kuwa mkataba wa Dowans haukuwa na tofauti kubwa na mkataba wa Richmond na Tanesco. Sasa tayari tumeshajua kuwa hatuwezi kuwaamini hawa kwanini leo tugeuka na kutaka kuwapa watu hawa hawa mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania, kwa umaskini gani tulionao?



Ngeleja

d. Watu wengi wasichokumbuka ni kubadilika toka Dowans Holding kwenda Dowans Tanzania Limited. Baada ya kugundulika kuwa kampuni ya Dowans Holding ina matatizo ya kisheria watalaamu wetu wakaamua kubadilisha na kuiita Dowans Tanzania limited ili angalau ionekane ni kampuni ya Watanzania na sitoshangaa kuwa kwa Tanzania ina wamiliki wazalendo. Hawa ni kina nani? Kwanini kubadilisha hivyo walikuwa wanaficha nini? Yawezekana hicho tulichokisema kwenye kifungu (b)?

4. Jaribio dhaifu la kuizunguka sheria ya manunuzi ya mwaka 2004

Kitu kimoja ambacho kimetushangaza sana ni jinsi gani serikali na wizara ambayo iliamua kuvunja mkataba wa Richmond na wa Dowans kutokana matatizo ya kisheria kuwa ndiyo watetezi wa kuizunguka sheria hiyo tena. Katika mahojiano na Mwanakijiji.com Waziri wa Nishati na Madili alisema kuwa safari hii serikali haijatangaza zabuni kwa sababu ni Dowans ndiyo wanataka kuuza mitambo yao na kuwa ni wao wametangaza zabuni.
Zabuni ya Dowans ilitangazwa mwishoni mwa mwaka jana (tunaamini

Soma bure

TUNASEMA HAPANA KWA DOWANS!

mwisho wa mwezi wa kumi au mapema Novemba). Kwa mujibu wa jarida la kimataifa la Africa Intelligence uamuzi huo "lilikuwa ni chagua pekee walilobakia nalo Dowans baada ya serikali kuvunja mkataba" mwezi wa nane.

Walipoanza kuzungumza suala la kununua majenereta ya Dowans mapema mwaka huu kulikuwa na upinzani mkali na hatimaye serikali ikarudi nyuma. Mwezi wa tatu tena suala hili linakuja tena kwa nguvu zaidi na safari hii kwa kuchezea hisia za uzalendo wa Taifa. Kwamba, tusiponunua majenereta hayo basi hatuitakii nchi mema au tunakosa uzalendo.

Kwanini? Tunaamini kuna sababu kubwa mbili ambazo zimeleta msukumo huu. Kwanza, tangu Dowans watangaze tenda yao hakuna kampuni yoyote wala mfanyabiashara yoyote mwenye akili timamu aliye tayari kulipa shilingi bilioni 60 na zaidi kununua majenereta haya! Sababu ya pili, kwa kufikiria kuwa kwa vile Dowans ndiyo wenye tenda basi serikali haifungwi tena na sheria ya tenda na hivyo na wenyewe watakuwa kama wanunuzi wengine sokoni kwenda kushindanisha bei na muuzaji.

Tunajiuliza, kama mnunuzi mwenyewe ni mmoja, na bidhaa iliyopo ndiyo hiyo peke yake, ni kwanini basi muuzaji aiuze bidhaa yake kwa bei rahisi wakati anajua mnunuzi anaiihitaji na yuko tayari kulipa kiasi chochote? Zaidi ya yote kwa vile tumeshatishiwa kuwa kutakuwa na "giza"

SWALI LA WIKI:

Tumejenga hoja juu ya kampuni ya Dowans, hata hivyo serikali bila ya shaka itaendelea kutekeleza adhma yake hii kwani kutotekeleza mpango huu kutaisababishia kampuni ya Dowans hasara kubwa ya kifedha.

Je wewe unajali?

majibu yako: **mhariri@klhnews.com**

muda si mrefu basi mnunuzi si atabakia anajichekelea tu kwani anajua mwisho wa siku mnunuzi atalazimika kumpigia magoti na tena anaweza akamuuzia bei ya juu zaidi?

Tuseme wazi kwamba sheria ya manunuzi ya serikali haitoi nafasi kwa chombo au idara yoyote ya serikali kununua kitu au kukiachilia kitu cha mali ya umma bila ya kuhusisha bodi ya tenda. Sheria hiyo ya PPA inasema wazi kuwa hakuna idara au chombo chochote cha serikali kitakachoingia mkataba mpaka mkataba huo uwe umekubaliwa na bodi ya tenda (31:1-3).

Kwa kitendo cha Tanesco kutaka kununua mitambo hii kama vile wanaenda sokoni wakati wao ndiyo wanunuzi pekee ni uvunjaji mkubwa wa sheria. Kama kweli serikali inataka value for money, utawala bora na kutokuwa na upendeleo, wao ndiyo waitishe tenda, kwa masharti yao, kwa vigezo vyao na waache kina Dowans na makampuni mengine yashinde kwenye jukwaa huru. Tunachokiona hadi hivi sasa ni jaribio la wazi la kuivunja sheria, kuibeba Dowans na kuizawadia mabilioni ya watoka jasho wa Tanzania.

Kwa sababu hii tunapinga Dowans!

5: Serikali isivunje kanuni ilyoziweka yenyewe.

Sheria ya manunuzi ya serikali inasomeka pamoja na kanuni za manunuzi ya serikali (2005) zilizotangazwa kwenye gazeti la serikali (GN No. 97). Kifungu cha 58:3 cha kanuni hizo kinasema wazi kuwa "Motor vehicles, heavy plant and spare parts to be purchased shall be brand new"

Sasa hoja hapa imetolewa kuwa hizi ni "kanuni tu". Tunaamini kuwa kanuni hizi siyo za kuchagua au kuacha (optional) ni kanuni zenye msingi wa kisheria na zinatakiwa kufuatwa. Msimamo huu unakuja tunaposoma sheria mama ya Manunuzi ya Serikali Ibara ya 17:1 ambayo inatoa adhabu kwa mtu yeyote au afisa yeyote ambayo inaiagiza Mamlaka ya Tenda kupendekeza hatua kuchukuliwa hatua kwa mtu yeyote ambaye ataonekana kuvunja "sheria hii au kanuni na miongozi inayotokana na sheria hii". Kwa maneno mengine, Dr. Idris Rashid na wenzake hawawezi kuagiza kununuliwa kwa mitambo chakavu kinyume cha kanuni.

Endapo watafanya hivyo, hatua zitachukuliwa dhidi yao miongoni mwao ni pamoja na kufukuzwa kazi!

Kama kununua vitu chakavu ni mojawapo ya kanuni zinazoruhusiwa kwanini serikali isiwaagizie watendaji wake magari mitumba badala ya mapya? Kama kanuni hizi ni mapendekezo tu ambayo wanunuzi wa serikali wana hiari ya kuzifuata au kutozifuata, sasa kuna ulazima gani kuwa nazo?

Kwa sababu hii tunaikataa Dowans.

Tunazo na sababu nyingine nyingi lakini hizi tunaamini zinatosha kutoa msimamo kuwa uamuzi wa kununua majenereta siyo sahihi, unastahili kupingwa na ni lazima kupingwa. Hata hivyo kabla hatujatoa wito kwa wasomaji wetu kushiriki katika kupinga mpango huu hatuna budi kutoa mapendekezo ya nini kifanyike kukabiliana na upungufu wa nishati ya umeme.

Kwanza, kutatua tatizo la nishati kukidhi mahitaji ya sasa hivi serikali iharakishe kuunganisha umeme wa Zambia katika gridi ya Taifa. Tanesco wenyewe wanasema kuwa umeme wa Zambia ukiunganishwa kwenye gridi ya Taifa kiasi cha Megawatts 200 zinaweza kuingizwa, hadi hivi sasa hatujui mradi huu umefikia wapi au nini kinasubiriwa kufanyika. Mradi huu unakisiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 170.

Maana yake ni kuwa badala ya kutumia bilioni 70 kununua majenereta ya Dowans kupata karibu Megawatts 120 hivi, ni bora kuunganisha umeme wa Zambia na gridi ya Taifa. Fedha pia tunajua zitakakotoka, kwenye mradi wa vitambulisho ambapo serikali inataka kutumia bilioni 200! Ukimuuliza Mtanzania kati ya kitambulisho na umeme kipi kifanyike kwanza atakuambia umeme! Hii nayo ni sababu nyingine ya kusitisha mradi wa vitambulisho.

Serikali iache kusuasua kuanzisha mradi wa Stiglers Gorge. Huu ndio mradi pekee ambao kwa asilimia 100 utahakikisha Tanzania inaondoka na tatizo la umeme daima. Tan-

Soma Bure
hoja zenye nguvu

HAPANA KWA DOWANS!

zania hatuhitaji umeme wa Nyuklia au wa mafuta, tuna maji ya kutosha kabisa ambayo tukiamua kweli tunaweza kuwa huru katika suala la nishati. Huu mtindo wa kulipa milioni 50 hapa, milioni 30 pale ni upotevu mkubwa wa fedha za umma na wakati umefika viongozi wetu wakomeshe.

Tunahitaji uongozi wenye maoni, dhamira ya kweli, na ujasiri wa kuanza kutekeleza mradi huu kama vile Wachina walivyofanya kwenye mradi wao wa maporomoko matatu ambao ndio mradi mkubwa kabisa wa umeme wa maji duniani. Wa kwetu utakuwa ni kiduchu tu lakini tukiukamilisha tutakuwa na umeme wa kutosha kwa matumizi ya ndani (viwanda na makazi) na kuuza mwingine kama ziada. Wakati wa kuutekeleza mradi huu umefika.

Wito wetu kwa kwa wasomaji wetu ni kuonesha kuwa hawaridhiki na hawako tayari kuona fedha zao zinapelekwa kwa Dowans na ya kuwa hata kama itabidi wananchi ambao tayari hawana umeme wakose umeme kwa muda hata wa mwaka mmoja basi iwe hivyo kuliko kuwapa Dowans fedha hizo.

Tunatoa wito kwa wasomaji wetu kumpigia simu waziri wa Nishati na Madini Mhe. William Ngeleja na kumuambia kuwa asiendelee kuutetea mpango wa kununua majenereta ya Dowans bali aongoze wizara kutafuta vyanzo vingine kwa tenda. Pia, tumhakikishie kuwa kuliko kupoteza fedha hizi kwenye mradi huu ni vizuri fedha hizo zianze kutengwa ili hatimaye tutekeleze mradi wa kuunganisha na Zambia (kuondoa tatizo la wakati huu) na pia mradi wa Stielgers.



Pamoja na Waziri Ngeleja ujumbe huo huo tuutume kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco Dr. Idris Rashid na kumuambia na yeye aachane na mpango huo na asitumie nafasi yake kuwabeba rafiki zake. Unaweza kupiga au kutuma sms isemayo "Msiwazawadie Dowans fedha za jasho letu, tangazeni tenda mwenye kushinda ashinde – say NO".

Namba ya **Mhe. William Ngeleja** ni: **754 710070**

Namba ya **Dr. Idris Rashid** ni: **754 280 442**

Sisi Watanzania tunaweza kukaa pembeni na kulalamika au tunaweza kusimama na kuhamasika kuwakatalia. Tusiposimama kama ambavyo hatukusimama kwenye Rada ya bilioni 40 na ndege ya bilioni 50 ndivyo watawala wetu watakavyoendelea na wenyewe kuja na miradi ya aina hii. Wakati serikali hii haijamaliza hata kesi yao na Dowans, hawajamaliza kesi za EPA, hawajaana mambo ya Meremeta, hawajagusa suala la Deep Green, Mwananchi, na Tangold, na hawajajua matokeo ya kesi ya Minara Miwili wanarudi tena na kuja na mradi mwingine.

Aidha wanatudharau sana na kutuona duni, au wanaamini kuwa wananchi siyo kitu. Tunaamini yote mawili ni kweli. Tumedharauliwa vya kutosha, tumepuuzwa vya kutosha, na tumeburuzwa hadi tumechubuka. Tukiwakatalia hili, huko mbeleni watafikiria tena. Kuwakatalia kwetu si kwa sababu ya ugomvi au chuki; si kwamba tunawaona wote ni mafisadi, kuwaandikia ujumbe huu ni nafasi pekee ya wananchi kusikilizwa.

Vinginevyo watambue kuwa wale wote watakaoulazimisha mradi huu katika makoo ya Watanzania kwa kisingizio chochote kile wao wawe wa kwanza kuwajibika kwani tutahakikisha Bunge linafanya kile ilichofanya kwa wenzao ambao waliamini wanaweza kufanya lolote kwa Watanzania. Tunasema '"HAPANA DOWANS'!

DA' JESSY: TUKISHAWATAJA HALAFU?

Na. Jessica L Fundi

Naona tuseme ukweli tu. Viongozi wetu wanapenda kutafuta masuluhisho mepesi kwa matatizo au masuala magumu.

Kwenye hotuba yake ya mwisho wa Mwezi Rais Kikwete ameelezea juu ya utekelezaji wa jambo alilioliahidi miezi michache iliyopita kuwa wananchi wawataje wale wanaowatuhumu kuhusika na biashara na mauaji ya Albino.

Serikali yake imekuja na mpango wa kufanya hivyo kwa njia ya kura ya maoni ambapo watu watatoa maoni yao kwa usiri.

Inaonekana kuwa mtu yeyote mtaani ambaye atapata "kura nyingi" basi huyo atakuwa mmoja wa watuhumiwa wa mauaji na vyombo vya usalam vitamfuatilia kumchunguza au hata kumchukulia hatua.



Sijui ni nani aliyekuja na mapendekezo hayo au utaratibu huu wa kujaribu kutatua tatizo la mauaji ya kinyama ya Albino kwa njia ya kupiga kura.

Sasa, watakaoonekana kutajwa bila ya shaka watakuwa ni watu ambao ni matajiri. Wale ambao wamepata utajiri wao baada ya kuhangaika sana au kufanya kazi na sasa wanavuna matunda watajikuta wanatajwa kwa sababu hawatakuwa tayari kuwaambia watu siri za utajiri wao bila kufichua siri za biashara.

Matokeo yake, serikali itaanza kutengeneza kundi jingine kabisa katika jamii ambalo nalo maisha yake yataanza kuwa hatarini. Hawa watakuwa ni watu wale ambao watatajwa katika kura hizi za maoni.

Sioni ni jinsi gani "baba Junior" atasalimika au rafiki zangu watasalimika. Sielewi ni kwa jinsi gani kundi la watu wenye kisasi cha biashara au wenye wivu watazuiwa kupandikiza mbegu za chuki dhidi ya mtu fulani.

Kura za maoni zinaweza kuwa nzuri kwenye mammbo fulani hasa ya kisiasa na yenye kuhitaji maamuzi ya jamii. Linapokuja suala la uhai wa watu na uhuru wa maisha yao kutegemea kura hizi kuwa zitatenda haki ni kuweka hatarini maisha yale ambayo tunataka kuyalinda.

Sasa tukishapiga hiyo kura halafu nini?

Email: dajessy@klhnews.com


MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...


KATUNI ZA WIKI

Picha ya Wiki



Waliojifungua wakipumzika Hospitali Temeke





PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KUTOKA KWENYE MTANDAO

Mwanakijiji ahsante kwa mahojiano yako na Mh.Ngeleja ambayo kwakweli yanazua maswali kuliko majibu.Swali la kwanza ambalo mimi ningemuuliza serikali ilipovunja mikataba na hayo makampuni ya umeme aliyoyataja serikali ilikua alternative au mpango ngani wa kuziba mapengo yaliyoachwa na makampuni hayo? - **Advocate Jasha**

Dr Idrisa Rashid alikuwa kwenye dili ya rada na sasa Dowans mitambo.....hao watu wananuka rushwa kwa nini wanaendelea kupewa madaraka bila kuwajibishwa na pia kufikishwa mahakamani.....mimi nadhani jumuiya za kimataifa zisiishie kuwa tuu na mahakama ya kimataifa ya ualifu kivita, Tumefikia wakati sasa pia iundwe Mahakama ya mafisadi ya dunia ili kulindana kuishe maana hapa ni kulindana ndiyo kitu kikubwa ktk siasa za tanzania kwa sasa - **Kama**

Wanakijiji kama ni mgao wa umeme tumezoea tangu uanze rasmi 1992 huo udharura ni uchovu wa kufikiria wa viongozi wa tanesco ndio umetufikisha hapa tulipo. Mitambo ya dowans on wheels na LM 6000 ni ya zamani mno hata vipuri vyake kwa mbinde. SONGAS wanayo walirithi ile iliyonunuliwa miaka ile ya 90 na inawasumbua kinoma. Mbona wanaogopa giza wakati Watanzania 85% hawajawahi kuona huo umeme. Mbona juhudi za kuwasha mitambo ya Tegata 45mw NI KAMA ZA konokono?- **Mkereme**

Kuna mkono wa mtu, tena mkono wenyewe ni wa chuma, kwanini maamuzi yetu wenyewe tunayakanyaga, kama wanapinga, turudi bungeni– **Mhe. Lucas Selelii**

Sisi tunasema kama kununua wanunue, wameomba vibali mara ngapi, wananunua sijui nguzo!!! wamekuja lini kwetu. Naamini kwenye hili wamegundua kuna kitu hakiko vizuri ndio wanataka kuhalalisha.. Sisi tulitoa maoni, Tanesco ina ujanja wa aina fulani, sijui wanataka nini? - **Dr. Harrison Mwakyembe**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa– Mhariri

Freddy Katunzi–Habari za Siasa

Mahmoud Rashid–Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*